



**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**



TAARIFA KWA UMMA

**MAREKEBISHO YA TAREHE YA KUANZA KWA UUZWAJI WA KOROSHO GHAFI
KWA MSIMU WA 2026/2027**

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo, yenye dhamana ya kusimamia na kuendeleza Tasnia ya Korosho nchini Tanzania. Bodi ilianzishwa chini ya **Sheria ya Tasnia ya Korosho, Sura ya 203, Toleo la 2023**, pamoja na kanuni zake za mwaka 2010, ambapo majukumu yake ya udhibiti yameainishwa chini ya Kifungu cha 4 cha sheria hiyo.

Bodi ya Korosho Tanzania inawajulisha wanunuzi wote wenye leseni za korosho ghafi pamoja na wadau wengine kuwa tarehe ya kuanza kwa minada ya korosho ghafi kwa msimu wa 2026/2027, ambayo ilitangazwa awali kuwa ni tarehe 19 Oktoba 2026, imefanyiwa marekebisho.

Hivyo, minada ya korosho ghafi kwa msimu wa 2026/2027 itanza rasmi tarehe **12 Oktoba 2026**.

Wadau wote wanaohusika wanashauriwa kuzingatia marekebisho haya na kufanya maandalizi muhimu kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na masharti yanayosimamia ununuzi na uuzaji wa korosho ghafi nchini.

Ahsanteni kwa ushirikiano wenu.

**Imetolewa na:
MKURUGENZI MKUU
BODI YA KOROSHO TANZANIA
27 SEPTEMBER 2026**